# Mpeni Kaisari Vilivyo Vyake Kaisari

## (Na Mungu Vilivyo Vyake Mungu)

**na**

**J. D. Logan**

# Mpeni Kaisari Vilivyo Vyake Kaisari

## (Na Mungu Vilivyo Vyake Mungu)

**na**

**J. D. Logan**

**Novemba 5, 2011**

# Mpeni Kaisari Vilivyo Vyake Kaisari

## (Na Mungu Vilivyo Vyake Mungu)

## Kifungu: Mk 12:14-17

Katika ulimwengu wa dini leo kuna mkanganyiko mwingi kuhusiana na wajibu wa kanisa na ile ya serikali katika maisha ya Wakristo. Jinsi gaini tunapaswa kutawaliwa na haki yetu ya msingi inaegemea wapi?

Je twapaswa kuangalia "mambo ya Kaisari" kwa ajili ya muongozo wa kiroho? Je mamlaka yamewekwa na Mungu ili kutunga sheria ya dini na tabia njema ambayo tunatakiwa kutawaliwa kwayo? Kimsingi nguvu za kidunia haziwezi kuzidi zile za Mungu, au sheria zao kutungwa kimakosa na kuwaongoza watu vibaya, iwe katika msukumo huo ambao tunaweza kuzitazama kwa ajili ya muongozo wa kidini.

Katika kifungu chetu, Bwana wetu alitaja jukumu la msingi kwa wafuasi wake kwa kuishi huku kuwili. Hakuonyesha uaminifu usio hojiwa kwa vyote. Tunatofautishaje kati ya mawili?

Kama ilivyo kawaida, tutachunguza maneno ya Bwana wetu na mitume wake kwa muongozo na siyo wanasiasa wanaojichagua au mnenaji wa hadhara anayeweza kunena badala ya Mungu.

## Uzao mteule

"*Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu; ninyi mliokuwa kwanza si taifa, bali sasa ni taifa la Mungu, mliokuwa hamkupata rehema, bali sasa mmepata rehema. Wapenzi, nawasihi kama wapitaji na wasafiri, ziepukeni tama za mwili zipinganzo na roho"* (1 Pet. 2:9-11)

- Uzao, "genos"… malimbuko, taifa, watoto, mali" (1085 – Strong).
- Taifa, "ethnos"…kabila, taifa, watu, kikundi" (1484, Strong)
- Watu, "laos"… "wale wote ambao ni wa kikosi kimoja na wananena lugha moja" (Online Gr. Lex.)
- Wageni, "paraikos"… "anayeisha ulimwenguni kama mgeni, wapitaji duniani. Ya Wakristo, ambao makao yao yako mbinguni."
- Wapitaji, "parepidemos"…mkazi wa kigeni" (3927 – Strong)

## Wenyeji

"*Kwa maana sisi wenyeji wetu uko mbinguni; kutoka huko tena tunamtazamia Mwokozi, Bwana Yesu Kristo.*" (Fil.3:20)

- Mazungumzo, "politeuma"…nchi, dola (la wenyeji)"; pia kuanzishwa kwa dola, uundwaji wa serikali na sheria ambayo inalindwa." (4175 – Strong).

## Watu wa kipekee

(Yesu Kristo) "*Ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote, na kujisafisha watu wawe milki yake mwenyewe, wale walio na juhudi katika matendo mema.*"

- Kipekee, "laos" watu, kikundi, kabila, taifa, wale wote walio wa kundi moja na kabila" (2992 – Strong).

Kwa ufupi, Petro anasema kuwa sisi ni watu wa kipekee (wake) katika ukuhani na utaifa wa umoja wa kimbingu ambao mkuu wao yuko mbinguni.

## Sheria za kimbingu

"*Yesu akajibu, akamwambia mtu akinipenda, atalishika neno langu na Baba yangu atampenda; nasi tutakuja kwake, na kufanya makao kwake.*" (Yohana 14:23)

Kristo kichwa chetu, anayetawala kutoka mbinguni, ni mwanzilishi wa sheria zinazo waongoza watu wake. Katika safari yake yote ulimwenguni, alirudia kusisitiza umuhimu wa neno lake kama sheria kwa watu wake.

Neno la Bwana inaanzisha sheria ambayo tunapaswa kuegemeza uhusiano wetu katika maisha haya. "*Lakini mwenendo wenu na uwe kama inavyoipasa Injili ya Kristo……..*". (Fil.1:27).

- Mazungumzo, "politeuomai" kuwa na taifa…kudumisha binafsi au kutambua sheria (4176 – Strong).

## Mitume

Paulo alieleza wazi wajibu wa mafundisho ya mitume katika uhusiano wa ufalme wa mbinguni. "Mtu ye yote akidhani ya kuwa ni nabii, au wa kiroho, basin a akubali ya kuwa vitu niwaandikiayo ni agizo kutoka kwa Mungu." (1 Kor. 14:37).

Ni hivi, pia, kwamba tunaangalia muongozo katika mambo yote kiroho na si kwa sheria za wanadamu ambazo maranyingi uongoza watu vibaya.

## Kujitowa kwetu, uaminifu, wajibu

Kujitoa kwetu kote na uaminifu unaegemea wapi? Kwa Mungu au wanadamu? Jibu linapatikana katika neno lake. "*Hii ndiyo jumla ya maneno yote yamekwisha sikiwa; mche Mungu nawe uzishike amri zake. Maana kwa jumla ndivyo impasavyo mtu.*" (Wim. 12:13).

"*Akajibu akasema, mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako.*" (Luka 10:27).

Wenyeji wa ufalme wa mbinguni, sisi ni askari wa Mfalme na tunahitajika kutoa huduma ya nafsi zetu kwa Mkuu wetu.

"*Kwa kuwa ilimpasa yeye, ambaye kwa ajili yake na kwa njia yake vitu vyote vimekuwapo, alileta wana wengi waufikilie utukufu, kumkamilisha kiongozi mkuu wa wokovu wao kwa njia ya mateso.*" (Ebr. 2:10)

## Muogope Mungu na kumheshimu Mfalme

Kama "kama wajibu wetu wote ni kwa Mungu" je ni jukumu lipi tunalolichukua kwa wenye mamlaka ambayo tunaishi katika dunia leo hii? Lazima tutafsiri uwezo wa serikali za kidunia kama inavyoelekeza neno la Mungu.

"*Hukumu hii imekuja kwa agizo la walinzi, na amri hii kwa neno la watakatifu, kusudi walio hai wapate kujua ya kuwa Aliye juu anatawala katika ufalme wa wanadamu, naye humpa amtakaye, tena humtawaza juu yake aliyemnyonge.*" (Dan. 4:17).

Danieli alikuwa anshughulika na Nebuchadnezzar, Mfalme wa Babiloni, mtu aliyekuwa akijivuna na kujisifu. "*…Mfalme akasema mji huu sio Babeli mkubwa niliojenga mimi, uwe kao langu la kifalme, kwa uwezo wa nguvu zangu, ili uwe utukufu wa enzi yangu?*" (Dan. 4:30).

## Uaminifu unaopingana

Kuna matukio mengine ambayo "vitu vya Kaisari" (sheria ya serikali) ikipingana na vya Mungu (sheria iliyovuviwa). Je tufanye nini?

"*Petro na Yohana wakawajibu, kwamba ni haki mbele ya Mungu kuwasikiliza ninyi kuliko Mungu, hukumuni ninyi wenyewe; maana sisi hatuwezi kuyaacha kuyanena mambo tuliyoyaona na kuyasikia.*" (Mdo. 4:19-20)

Watawala wa Israeli walizuia uhubiri wa injili lakini Mitume wakakaidi kutii. Kiuwazi, hili lilikuwa ni swala la kutokutii maagizo ya serikali. Kunapokuwa pingamizi kati ya pande zote mbili, wajibu wetu ni kumtii Mungu, siyo mwanadamu!

## Mungu anatawala

Waziwazi, tunaweza kuona kwamba Mungu wa mbinguni ananguvu zote dhidi ya wanadamu, na anaruhusu wanadamu wa kawaida kuwa watawala katika mataifa yao, haijalishi wanaweza kuwa bora kiasi gain. Katika vitabu vyote vya Agano La Kale, tunakuta kwamba Mungu, kwa nyakati tofauti, alitumia udhaifu wa mataifa ilikuleta kuanguka kwa watu wake walioanguka kutoka katika mwongozo wake.

Wakati makabila 10 ya ufalme wa Israeli walipoingia zaidi katika uchafu, Mungu aliwahutubia wafalme wa Ashuru na Misri kutoa hukumu yake dhidi yao (angalia Isa. 7:17-20). Hakika Mungu anatawala katika ufalme wa kibinadamu!

Mungu ameweka mipaka (ukomo) wa mataifa ya binadamu na wakati wa utawala wao. "(Mungu)…*naye alifanya kila taifa la wanadamu kutoka katika mmoja wakae juu ya nchi yote, akiisha kuwawekea nyakati alizoziamuru tangu zamani, na mipaka ya makazi yao.* (Mdo. 17:26).

Nebukadneza maskini, alifikiri, kwamba alifanya utawala wote uliomzunguka, na akashindwa kutoa utukufu kwa Mungu, kwa ambaye ni mwenyewe, na ilimbidi ajifunze somo la gharama katika mlolongo huo.

## Masomo yetu

Sasa hii yote inamaanisha nini kwetu sisi leo, kama somo la jumuia ya Mungu wa mbinguni? Tuna muongozo wa wazi dhidi ya wajibu wetu katika mamlaka ya dunia ambayo tunaishi kwalo.

- Sisi ni wananchi wa ufalme wa mbinguni.
- Wageni na wasafiri katika dunia.
- Sheria ya Mungu inazidi ya kidunia.
- Tunapokuwa katika pingamizi, na sheria za Mungu, lazima tuache kumtii mwanadamu.

Maombi zaidi,

J D Logan